Pakua nakala hii ya PDF
kwenye www.jw.org/sw

Yosefu Katika Nchi ya Misri

MWANZO SURA YA 39-40

BAADA YA SAFARI YA SIKU NYINGI, YOSEFU AMBAYE ALIUZWA NA NDUGU ZAKE KAMA MTUMWA, **HATIMAYE ALIWASILI MISRI.**

EEH, **POTIFA,** UTAMNUNUA AU LA?

YEYE NI **KIJANA** NA **MWENYE NGUVU.** HAKIKA, NITAMNUNUA.

BAADA YA MUDA, YEHOVA ALIMSAIDIA YOSEFU KUWA MTUMWA MWENYE MAFANIKIO KATIKA NYUMBA YA POTIFA . . .

UMEFANYA VIZURI PIA KAZI HII YOSEFU!

ASANTE, BWANA WANGU. MUNGU WANGU, **YEHOVA,** NDIYE ANAYENISAIDIA.

www.jw.org © 2013 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania



www.jw.org © 2013 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania

POTIFA ALIPORUDI, MKE WAKE AKAMWAMBIA UWONGO.

. . . NA KISHA YOSEFU AKAJARIBU **KULALA** NAMI. LAKINI **NILIPIGA KELELE,** KWA HIYO AKAIACHA KANZU YAKE NA **KUKIMBIA.**

LAZIMA YOSEFU **AADHIBIWE!**

POTIFA AKAMTUPA YOSEFU **GEREZANI . . .**

LAKINI YEHOVA ALIENDELEA **KUMTUNZA** YOSEFU.

www.jw.org © 2013 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania

SIKU MOJA, YOSEFU ALIWAONA WAFUNGWA WAWILI AMBAO WALIKUWA WAFANYAKAZI WA **FARAO,** MFALME WA MISRI.

KWA NINI NYINYI WANAUME MNA **HUZUNI** SANA LEO?

TULIOTA **NDOTO.**

LAKINI HAKUNA MTU ANAYEWEZA KUTUAMBIA MAANA YA NDOTO ZETU.

NILIONA **MATAWI MATATU** YANAYOTOA **ZABIBU.** KISHA NIKAZIMINYA ZABIBU NDANI YA **KIKOMBE CHA FARAO** NA NIKAMPA.

MUNGU ANAWEZA KUWASAIDIA KUELEWA MAANA YA NDOTO ZENU. TAFADHALI **NIAMBIENI** NDOTO ZENU.

KATIKA NDOTO YANGU, **VIKAPU VITATU** VYA MIKATE VILIKUWA KICHWANI PANGU. LAKINI NDEGE WAKAANZA KULA **CHAKULA CHA FARAO** KILICHOKUWA KATIKA KAPU LA JUU.

NDOTO YAKO INAMAANISHA KWAMBA BAADA YA **SIKU TATU UTARUDI KUMTUMIKIA FARAO.** UTAKAPORUDI, TAFADHALI **UNIKUMBUKE** NA UMWAMBIE FARAO KUNIHUSU KWA SABABU NILITEKWA NYARA NA SIKUPASWA KUWA GEREZANI.

NDOTO YAKO INAMAANISHA KWAMBA BAADA YA **SIKU TATU** FARAO **ATAKUUA!**

SIKU TATU BAADAYE, WAKATI WA SIKUKUU YA KUZALIWA KWA FARAO, ALIMRUDISHA YULE MFUNGWA WA KWANZA ILI **AMTUMIKIE.** LAKINI FARAO **AKAMUUA** YULE MFUNGWA WA PILI.

WAKATI ULIPITA . . . NA YULE MFUNGWA ALIYEOKOKA **ALIENDELEA KUSAHAU** KUMTAJA YOSEFU KWA FARAO. LAKINI JE, **YEHOVA** ALIMSAHAU YOSEFU? JE, YOSEFU ATAWAHI **KUTOKA** GEREZANI? KATIKA HADITHI YA BIBLIA INAYOFUATA, ONA JINSI YOSEFU ALIVYOWEZA KUSAIDIA **FAMILIA** YAKE—NA **TAIFA** ZIMA!

TUNAJIFUNZA NINI KUTOKA KWA YOSEFU AKIWA NCHI YA MISRI?

KWA NINI YOSEFU **ALIMTII** YEHOVA HATA WAKATI ALIPOKUWA **MBALI** NA FAMILIA YAKE?
DOKEZO: METHALI 15:3.

KWA NINI YOSEFU **ALIKIMBIA** MKE WA POTIFA ALIPOJARIBU KUMWINGIZA YOSEFU KWENYE DHAMBI?
DOKEZO: MWANZO 39:9.

TUNAPOPATA **MAFANIKIO** AU TUNAPOKUWA NA **UWEZO** WA PEKEE, TUNAPASWA **KUKUMBUKA** NINI?
DOKEZO: MWANZO 39:3, 23; 1 WAKORINTHO 4:7.

www.jw.org © 2013 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania